



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
WIZARA YA AFYA, USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO.**

**MUONGOZO WA UTOAJI HUDUMA KWA WAGONJWA NA WAHISIWA WA
UGONJWA WA KORONA (COVID-19) KWENYE VITUO VYA AFYA NA HOSPITALI
ZANZIBAR**

TOLEO LA PILI: 05 JULAI 2021.

UTANGULIZI

Kutokana na mwenendo tulionao sasa wa maradhi ya COVID-19 ulimwenguni na ujio wa hali ya hatari ya wimbi la tatu la virusi vinavyosababisha maradhi hayo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya, Ustawi Wa Jamii, Wazee, Jinsia Na Watoto imeamua kuongeza nguvu na kuimarisha hatua za kimkakati wa kinga na tiba dhidi ya ugonjwa huu.

Kwa muktadha huo kila kituo cha afya na hospitali zinatakiwa kuhakikisha zinatekeleza yafuatayo:

1. Wafanyakazi wote wanapaswa kuvaa barakoa wakati wote wakiwa katika mazingira ya kazi na si utaratibu wa kazi kutoa huduma kwa mgonjwa bila kuvaa barakoa.
2. Wananchi wote wanaoingia hospitali au kituo cha Afya wanatakiwa wavae barakoa wakati wote na hawatoruhusiwa kuingia ndani ya Kituo cha afya/hospitali bila kuvaa barakoa.
3. Kituo cha Afya na hospitali zinatakiwa kuhakikisha uwepo wa vifaa vya kunawia mikono vyenye maji tiririka na sabuni au vitakasa mikono kwa ajili ya usafi binafsi wa watoa huduma na wananchi wote wanaoingia maeneo ya hospitali au kituo cha Afya
4. Kituo cha afya na hospitali zinatakiwa kutenga eneo maalum la kufanya ukaguzi (screening), na upembuzi (triage) wa wagonjwa na watu wote wanaoingia maeneo ya kituo cha afya na hospitali kwa kufuata miongozo inayotambulika na kukubalika nchini, ili kuibua visa zaidi na kuzuia kuenea kwa maambukizi
5. Hospitali na vituo vya afya, zinatakiwa kufuata mtiririko mzuri wa kutenganisha wagonjwa au wahisiwa wa COVID 19 na wagonjwa wenye magonjwa mengine ili kuepusha maambukizi na kutoa kipaombele cha matibabu kwa wagonjwa au wahisiwa wa COVID 19.
6. Kuwepo na sehemu maalum au wodi kwa ajili ya kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa wa COVID 19. Sehemu hiyo inatakiwa iwe na hali nzuri ikizingatia uwezo wa kupitisha hewa safi kama inavyoshauriwa na wataalamu wa afya.

7. Pasiwepo na ubaguzi au unyanyasaji wa mgonjwa yoyote wakati wa kupokelewa na kupewa huduma
8. Wafanyakazi wa vituo vya afya na hospitals wanatakiwa wafate utaratibu wa rufaa kwa wagonjwa kama inavoelekezwa katika miongozo ya wizara ya Afya bila ya kuathiri utoaji wa huduma wakati mgonjwa akisafirishwa kutoka kituo kimoja kwenda chengine.
9. Mgonjwa aliezidiwa na mwenye sifa za kupata rufaa kwenda kwenye kituo chengine ambacho atafaidika na utofauti wa huduma za tiba zinazopatikana huko hahitaji kusubiri kipimo cha COVID 19, apewe rufaa na kipimo hicho kitatolewa katika kituo kitakachompokea ili kuepusha ucheleweshaji wa huduma zitakazomsaidia kuepusha matatizo zaidi/ulemavu wa kudumu au kupoteza maisha.
10. Kwa wagonjwa walioruhusiwa kwenda kujitenga nyumbani kuwe na utaratibu maalum ufatiliaji kutoka kwa wataalam wa afya wilayani na vituo vya matibabu husika.
11. Vituo cha afya na hospitali vinatakiwa kuweka kumbukumbu na kutoa taarifa sahihi za mwenendo wa maradhi ikiwemo idadi ya wahisiwa, waliothibitika, waliochukuliwa sampuli kwa uchunguzi kila siku kwa kufuata muongozo wa utoaji taarifa za maradhi ya mripuko.
12. Utoaji huduma kwa wagonjwa wa COVID 19 na taratibu zake zitafuata miongozo iliyoandaliwa na inayoendelea kutolewa na wizara ya Afya Zanzibar.
13. Taarifa za wagonjwa zitaendelea kutolewa kwa kufuata utaratibu uliopo kwa kumhusisha mganga mkuu wa wilaya husika.
14. Kituo cha kutolea huduma kifanye uchambuzi (death audit) kwa kila kifo kinachotokea na kinachohusiana na maambukizi ya COVID 19.
15. Endapo mhisiwa atapoteza maisha, sampuli ichukuliwe mapema iwezekanavyo, mwili uandaliwe kwa kuzingatia muongozo wa kulinda na kuinga maambukizi. Aidha ndugu wa marehemu wakabidhiwe maiti pamoja na kupewa maelekezo ya tahadhari za kuchukua ili waendeleo na taratibu za mazishi.

Waganga wakuu wa wilaya, wakuu wa vituo vya afya/hospitali, wakuu wa vitengo na idara zinazohusika kutoa huduma za afya katika vituo vya afya/hospitali zote nchini za umma na binafsi, wanaelekezwa kusimamia utekelezaji wa muongozo huu ambao utaendelea kutumika mpaka hapo wizara/serikali itakapotoa maelekezo mengine.

Imetolewa na:



Abdullah S. Ali
Mkurugenzi Mkuu

Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar.